# Umuhimu wa mifumo ya masoko katika kupunguza pengo

**Ripoti ya UNEP ya Pengo la Uzalishaji ya mwaka wa 2021 inaonyesha kuwa uzalishaji wa gesi ya ukaa kila mwaka unahitaji kupunguzwa kwa nusu kufikia mwaka wa 2030 ili kudhibiti joto duniani lisizidi nyuzijoto 1.5, lakini Ahadi Zinazotolewa na Taifa (NDCs) chini ya Mkataba wa Paris bado hazitoshi. Makala haya yanaangazia jinsi mifumo ya soko inavyoweza kusaidia kushughulikia mazingira.**

## Kwa nini mifumo ya masoko ni muhimu?

Mifumo ya Masoko - ikijumuisha bei ya kaboni, udhibiti na biashara, na shughuli za hiari - inaweza kuwa sehemu muhimu ya mikakati mikuu ya kufikia malengo ya mda mrefu ya Mkataba wa Paris. Masoko yanaweza kutoa fursa kwa nchi, kampuni na wahusika wengine kufikia malengo yao ya kupunguza uzalishaji wa gesi chafu kwa gharama ya chini na kuimarisha malengo yao.

Idadi ya nchi ambazo - katika NDC zao mpya au zilizosasishwa - zimeonyesha mipango ya matumizi au uwezekano wa kutumia mbinu za ushirikiano kwa hiari, ikijumuisha masoko ya kaboni, imeongezeka karibu maradufu ikilinganishwa na NDC za awali.

Masoko ya kimataifa yanaweza kuleta mabadiliko kwenye uwekezaji wa mtaji na kuuelekeza kwa maeneo ya masoko. Kwa kufanya hivyo wanaweza kusababisha athari chanya kwa hali ya hewa, kwa ajira na kwa mizani mingine endelevu katika eneo husika. Kwenye COP26, mataifa yatajaribu kukamilisha kitabu cha kanuni za biashara za uzalishaji wa gesi chafu chini ya kifungu cha 6 cha Mkataba wa Paris.



## Uwezo wa mifumo ya masoko ni upi?

Tayari kuna uzoefu wa kutosha katika kubuni na kutekeleza mifumo ya masoko ili kudhibiti vichafuzi, ikijumuisha aina mbalimbali za masoko ya kaboni. Hali ya sasa ya masoko ya kaboni ni anuai. Inajumuisha programu zinazoendeshwa kwa hiari na ridhaa na hutumiwa ndani na nje ya nchi kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, huku kukiwa na aina tofauti za marupurupu na mikopo na kushiriki kwa vyombo vya umma na sekta binafsi kama wanunuzi na wauzaji.

Tafiti za kimataifa zinakadiria kuwa, ikiwa NDC zote zitabadilishwa kuwa biashiara ya kukomesha uzalishaji wa gesi chafu na ikiwa nchi zote zitakuwa na malengo ya uchumi wote, basi karibu 4-5 GtCO2e inaweza kuuzwa kwa mwaka katika mwaka wa 2030.

Ikiwa akiba kutoka kwa utekelezaji wa NDCs kwa gharama nafuu ulimwenguni itatumiwa tena kuimarisha juhudi, uzalishaji wa gesi chafu unaweza kupunguza maradufu kwa muongo mmoja ujao bila gharama yoyote kuongezeka, ikilinganishwa na nchi zinazofanya kazi peke yake kutekeleza ahadi zao.

## Mifumo ya masoko inawezaje kufanya kazi?

Masoko ya kaboni yanaweza kupunguza uzalishaji halisi wa gesi chafu na kuimarisha juhudi, ila tu iwapo sheria zitafafanuliwa wazi, zibuniwe ili kuhakikisha kuwa shughuli zinazoendeshwa zitaweza kupunguza uzalishaji halisi wa gesi chafu, na zinasaidiwa na mipango ya kufuatilia maendeleo na kuweka wazi.

NDC zilizopo zina sehemu tu kidogo ya malengo ya uchumi yanayoweza kupimika, hali inayofanya kuwa vigumu kuanzisha mfumo dhabiti wa masoko duniani.

Sheria na muongozo unaoeleweka wa kifungu cha 6 unapaswa kufikiwa kwenye COP26, ili kuanzisha soko la kimataifa na kisha kulipanua polepole na kuliimarisha huku ahadi zinapoendelea kubadilika na maarifa kupatikana.

**Kuwezesha masoko kutekeleza majukumu dhabiti katika mchakato wa kukomesha uzalishaji wa gesi chafu, shughuli za sekta, gesi, na uchumi sharti zijumuishwe na kuweza kupanua masoko na kuyawezesha kufanya kazi kikamilifu.**



UNEP DTU PARTNERSHIP

UN environment programme 50 1972-2022